



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO



Kumb. Na SUA/ADM.A.1/9 Vol. VII/107

Tarehe: 15.09.2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Makamu Mkoo wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Morogoro, akishirikiana na Mkoo wa Jeshi la Polisi Tanzania anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wote wenye sifa za kujaza nafasi tatu (3) za ajira za Askari Wasaidizi kama zinavyoainishwa katika tangazo hili.

1.0 AP – KONSTEBO (NAFASI 3)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha nne au cha sita na amehudhuria na kutunukiwa cheti cha Mafunzo ya Askari Polisi Wasaidizi yanayotolewa na Vyuo vinavyotambulika na Jeshi la Polisi Tanzania.

2.0 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kusaidia katika kudumisha amani na usalama chuongi;
- ii. Kulinda mali za Chuo;
- iii. Kusaidia katika ulinzi wa maeneo nyeti ya Chuo;
- iv. Kusaidia katika kuwaongoza na kuwaelekeza wageni wa Chuo;
- v. Kusaidia katika kusindikiza mali za thamani za Chuo hadi mahali palipopangwa;
- vi. Kufanya kazi nyingine yoyote inayohusiana na ulinzi kama itakavyoagizwa na msimamizi.

3.0 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa mujibu wa Waraka wa Msajili wa Hazina Na.6 wa 2022 unaotumika kwa sasa.

4.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 25.
- ii. Maombi yote yaambatishwe na nakala ya cheti cha Mafunzo ya Askari Wasaidizi, cheti cha kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma hawaruhusiwi kutuma maombi.

- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayo jitoshela (Detailed C.V) yenyenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
 - v. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na NECTA.
 - vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
 - vii. Watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- 5.0 **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyo sainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Hati za matokeo za kidato cha nne/sita (FORM IV/VI RESULTS SLIPS) na Hati za viapo vya kuzaliwa (AFFIDAVIT) HAZITAKUBALIWA. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa Naibu Makamu Wa Mkuu Wa Chuo (Mipango, Fedha Na Utawala) S.L.P. 3,000 Morogoro. Mwisho wa kutuma maombi ya Kazi ni tarehe 29.09.2022

Imetolewa na



Prof. Amandus Pacificus Muhairwa
KNY: MAKAMU WA MKUU WA CHUO